UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu: 202-884-1080
202-939-6125
Nukushi: 202-797-7408
Barua pepe: ubalozi@tanzaniaembassy-us.org

1232 22nd Street, N.W.,
WASHINGTON, D.C. 20037

Kumb. Na. KBA 183/522/01 **27 Septemba 2016.**

Wenyeviti/Makatibu,
Jumuiya za Watanzania,
MAREKANI.

Yah: **MICHANGO YA HIARI KWA AJILI YA WAHANGA WA TETEMEKO LA ARDHI- KAGERA**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Kama mnavofahamu mnamo tarehe 10 Septemba 2016 Taifa letu lilikumbwa na janga la tetemeko la ardhi ambalo liliathiri kwa kiwango kikubwa sana Mkoa wa Kagera.

Ili kuonyesha mshikamano wetu wa kuwajali wenzetu waliokumbwa na maafa hayo, Watanzania kwa ujumla wetu, tunaombwa kuchangia kwa hali na mali ili kutimiza azma ya kuwawezesha wahanga wa tetemeko hilo kurudia hali yao ya maisha ya kawaida kama ilivyokuwa hapo awali.

Tunaomba michango hiyo iwasilishwe katika Akaunti rasmi ya kuchangia kama ifuatavyo:

JINA LA AKAUNTI:	**KAMATI MAAFA KAGERA**
AKAUNTI NA:	**0152225617300.**
SWIFT:	**CORUtztz**
JINA LA BENKI:	**CRDB Bank Bukoba**

Tunashukuru kwa ushirikiano wako

Dismas A. Assenga

Kny. **BALOZI**